KIBEKA

Muddyb Mwanaharakati

Dar General Publishing House

Kimechapwa na,
Dar General Publishing House,
Dar es Salaam,
Tanzania.
Mobile: 0713538427

Mhariri: Mwl. Eric Gamba
Mobile: 0767-839-430
Msanifu kurasa: Muddyb Mwanaharakati
Jalada: Frank Masai
Mobile: 0623-329-822

ISBN: 978-9976-5467-5-0
© Muddyb Mwanaharakati, 2020
Mobile: 0713-538-427
Chapa ya kwanza, 2020

Haki zote zimehifadhiwa.
Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kuuza, kupiga chapa, au kukitoa kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile bila idhini ya kimaandishi kutoka kwa Muddyb Mwanaharakati.

3 KIBEKA

MLANGO WA KWANZA

Mateso

Jua kali la saa nane lilicharaza ngozi ya kijana Kibeka aliyekuwa anakaribia kufika kwao. Ngozi yake iling'arishwa kilazima na michirizi ya jasho iliyokuwa ikipasua maungo yake. Hakuwa na leso wala kitambaa badala cha kujifuta. Zaidi alitumia kiganja cha mkono wake wa kuume kujifuta jasho hilo. Miguu yake ilishambuliwa mno na vumbi mithili ya mtu aliyejipaka saruji miguuni. Kiatu chake kimesheni uhaba wa kiwi kwa kitambo kirefu. Mwendo wake ulisema yote kama kachoka kupita maelezo. Mdomo mkavu, nywele zimetimka, shati haling'ai, bukta ya shule nayo uhai wake unaelekea ukingoni.

Alitembea hadi eneo la baraza yao, akaketi nje kwanza kujipumzisha kwa dakika kadhaa. Mkoba wa shule kando yake na chupa ya maji. "Ahsante, Mungu! Hatimaye nimefika nyumbani," alisema huku akikalia bungubungu. Hakuweza tena kukaa sawa kutokana na uchovu. Barazani kwao kuna kipande kikubwa tu cha kuweza kukaa ukapitiwa na usingizi. Juu kuna paa lililonakshiwa vizuri na bati la migongo mipana—msauzi, kivuli kizuri. Kilimkinga na kumsahaulisha kadhia ya juu kali lililomfukuza hivi punde. Kidogo akatopea usingizini bila kutarajia. Safari yake hiyo haikufika kokote ilifuatiwa na konzi lililotua kichwani mwake kutoka kwa mama'ke mdogo anayeishi naye hapo kwao.

4 KIBEKA

“Amka, kengemaji we’!” alisema kwa hasira huku akimkata jicho lililojawa na husda. “He! Mbona umenyorodoka hivyo? Una wazimu we’ mtoto eh?” mama mdogo aliongeza. Kijana hakujibu. “Ni jibu imekuwaje hiyo miguu kama umetoka kucheza ngoma?” mama mdogo aliendelea kumsakama kwa maneno kijana huyo. Akaona haitoshi, akamwinua kwa nguvu kidako mkingise bila kupenda. “Sa’ kama ni jeuri, mi’ nd’o kuhani wa ujeuri. Kuja hapa!” akaongeza kwa hasira huku akisafirisha mkonowe ukatua katika shavu la kulia la Kibeka. Hakulia wala hakutoa ukelele wowote ule. Jambo lililomkera sana mama’ke mdogo. “Wajitia nunda ama sivyo?” aliendelea kuhaha kwa maneno mithili ya mtu aliyenyimwa mgao pesa za kufungia upatu za mwishoni mwa mwaka. Katika kutaka kuondosha hiyo kadhia, Kibeka akajibu, “Nilichelewa kutoka shule gari likaniacha. Sikuwa na pesa tena ikabidi nitembee,” jicho alilotupiwa na mama’ke huyo—la haula! Si jema. “Ulikuwa wapi hata gari likakuwacha?” ma’ mdogo alifoka. Kibeka akamtazama kwa unyonge mtesi wake. Akasema.

“Nilienda kujisaidia kidogo chooni. Tumbo lilinisumbua sana,” akatulia kusikilizia nini kitatokea baada ya jibu lake. “We’ Kibeka una matatizo makubwa sana. Unapenda *kulakula* vitu vya ovyo nd’o maana unasumbuliwa na tumbo,” akamaliza na sonyo kali. “Nenda kabadilishe nguo zako,” alimsindikiza na konde la mgongoni. Pigo lilitoa sauti kali baada ya kutua mgongoni kwa Kibeka. Kwa taabu, akajizoazoa na kuanza safari ya kwenda ndani kubadili nguo. “Hiyo pesa yenyewe shi’ngapi hata ukasema *nakulakula* vitu ovyo,” Kibeka alisema akinong’ona—mama’ke asimsikie. “Umesemaje?” mama’ke alidakia *upesiupesi.* Akageuka kumsikiliza, akajibu.

5 KIBEKA

“Sijasema kitu mi’” akaendelea na safari yake. “Nyoo! Mshenzi mkubwa we’” ma’ mdogo aliendelea kumshambulia Kibeka aliyekuwa akipotea machoni mwake. Kibeka anasifika kwa ujeuri na kujibu watu. Haoni tabu kukushushuwa mbele za watu. Ni nani aliyemfundisha tabia hiyo? Endelea tu! Amekuwa mtu wa kupokea vipigo kila iitwapo leo. Hasa kutoka kwa mama’ke mzazi au mdogo. Anapata ahueni akiwapo bibi yake mzaa mama, Biti Tangatanga akiwa nyumbani. Kama akiwa mbali na mji, basi mkataba wa mateso wa kilazima unafungwa baina yake na hao anaowaita mama zake.

Biti Tangatanga ni kama jina lake, kutwa kiguu na njia kuzungukia mipango yake ya upatu, kutembelea ndugu na jamaa. Hajawahipo kukaa nyumbani japo wiki ikapita bila kuzua safari. Siku moja alipata kuulizwa na mfanyakazi mwenzake enzi hizo akifanya kazi katika kampuni ya kubangua korosho—TANITA.

“Hivi, Tangatanga—naona kila siku ukitoka kazini badala ya kwenda nyumbani, wenda njia tafauti kuzurura tena. Huchoki?” shogaye Tangatanga alimwuliza huku akibangua korosho na vicheko tele. “Shoga we’ acha tu. Jina hili mwenzangu linanieleleza tena. Kila kukicha kufuatilia madeni yangu ya khanga na vitenge nilivyokopesha nd’o ma’na unaniona situlii kila kukicha. Hata nikitulia n’takula nini? Mshahara wa TANITA wenyewe unaujua. Wame zetu wakiona tunawasaidia kulisha watoto nd’o wanapokuachia shilingi mia tano tena upike vyakula vinono. Vitoke wapi? Ukibisha utatafuta gubu lililolala. Siko tayari. Hakuna kitu ninachokipenda kama amani ya nausi yangu. Tabu hasa zinipitie mbali. Tunabembeleza ndoa na uzee huu tena nianze kutafuta yasotafutwa—kheri nijiepushe kwa kupita mbali kabisa eneo na lililokaribu na vilio vya majogoo ya jongomeo,”

akatulia. Shogaye akacheka. Biti Tangatanga ni mtu fulani wa maneno mengi na mwingi wa hikma.

“Kwa hiyo unataka kuniambia mumeo kakugeuza weye tena nd’o mtunza familia,” shogaye alisema akicheka. “Usiende huko. Nimepewa jina la Tabu Tangatanga. Hebu tazama kwanza mjina wenyewe. Ulitegemea mi’ ndo niltulie? Napambana tena na jina langu,” Biti Tangatanga alisema akicheka. Akainua mkono juu, akaurudisha chini kwa kasi, akapiga korosho, ikavunjika vibaya. “Imeyataka. Ilikataa pigo la kistaarabu,” Biti Tanga alisema. Shogaye tena alibaki akivunjika mbavu kwa kucheka.

***

Saa kumi na moja na nusu, aliamka akajiandaa *chapchap*, mkoba wake mgongoni. Akapita sebuleni, juu ya meza alikuta shilingi mia tano. Akaichukua na kuitia mfukoni. Akaenda jikoni, kuna meza ya kulia chakula iliyozungukwa na viti vinne vya mbao vilivyonakshiwa na foronya kubwa kiasi iliyobinjuka ndii. Rangi yake si njano wala nyekundu, lakini imependeza kwa ung’ao wake.

Kuna jokofu la milango miwili juu na chini. Jiko la umeme na gesi kando yake. Kabati za kuwekea vyombo zimepachikwa ukutani, ndani yake kuna mazagazaga mengi tu. Hakuhangaika na huko. Aliendea jokofu lilipo, akalifungua na kuchukua boksi la maziwa. Akaitwaa bilauri iliyokuwamo ndani ya kabati la ukutani juu, na kujimiminia. Akapiga funda la kwanza refu, akatua.

Akawa anasikilizia namna yalivyokuwa yakishuka tumboni kwake. Akapiga funda la pili refu vilevile kisha akatikisa kichwa. Kwa yakini utamu ulimkolea. Akainua tena kwa mara ya mwisho, bilauri ilirudi chini ikiwa tupu. Akataka kuongeza tena, lakini zoezi

lake likaishia njiani. Hamaki! Kofi moja mujarabu lilituwa kichwani kwake. Akageuka kumtazama aliyempiga.

“Mamaa!” alikuwa mama’ke mzazi. Akarusha lingine lakini akakwepa upesi. Akasogea mbele hatua mbili ili kutafuta usalama wake. “Uroho tu asubuhi-asubuhi. Ondoka hapa wende shule,” mama’ke alifoka. “Sa’ mi’ njaa inaniuma!” Kibeka alijibu huku akijikuna pale lilipotua kofi. Alipapasa shavu lake taratibu akisikilizia maumivu mithili ya mtu ajaribuye pasi kama inashika moto au la. “Dokodokoo!” mamaye alisema akibana pua. “Hebu nitokee hapa!” akaongeza akimsogelea.

“Utakula shule ukfika. Si tunalipia usafiri hadi chakula? Shenzi we’” aliendelea kufoka pasipo kunyamaza. “Chakula hadi saa nne sa’ n’takaa na njaa muda wote huo?” Kibeka alimjibu mama’ke kiudeko. “Nyamaza! Mbuzi kasoro mkiya we’” mama alisema huku akitaka kumchapa kofi lingine. Kibeka akakwepa na kutoka nje. Akaketi kibarazani akisubiri gari la shule limpitie. Akatoa kitana chake kidogo, akaanza kuweka sawa nywele zake. Akatoa tai yake aliyoiweka katika kifuko kidogo cha mkoba wake upande wa kushoto, akaifunga segemnege, tuli anasubiria kudura tena. Ilipotimu saa kumi na mbili na dakika kumi na tano, gari lilisimama mbele yake. Akakimbilia mbio, ndani. Kimya!

Hakusemeshana na mtu yeyote hadi anafika shule. Bado mawazo yake yalikuwa mbali sana akififikiria maisha anayoipitia kila siku. Kama hajateswa nyumbani, basi shule. Kipindi hiki bibi yake kasafiri huwa cha mateso sana. Nafsi yake ilikosa pumziko, hekaheka kila wakati. Usiku hakulala na asubuhi hakutamani kuamka. Kuna wakati aliaminishwa kuwa muda suluhisho la kila tatizo, yaani, ipo siku mateso yatakwisha. Ajabu ni kwamba hapendwi na mama yake mzazi, kwa hila iliyokosa izara, akawatia

sumu na ndugu wanaomfuata mama yake. Wakati mwingine alitajitahidi asiangalie saa iliyopo ukutani akiadhani pengine masaa yangeenda haraka zaidi. Wapi? Mateso juu ya mateso.

Jicho dirishani, mara chache angetazama sura za wenzake jinsi zilivyosheheni shamrashamra za uwepo wa furaha. Kila siku huwa anajiuliza furaha au raha ya maisha ni nini? Wapi alipowahi kukosea hata akaingia mtegoni mwa mateso namna hi?

Chozi likamtoka. Hata marafiki zake ni wale wanaosoma shule za watu wa chini. Hii shule ya kulipia anayosoma yeye hana hadhi nayo kutokana na wajihi wake. Anakumbuka mateso ayapatayo kila akiuliza habari za baba yake. Hakuwahipo kupata majibu yanayomridhisha. Mama'ke hujinasibu kuhusika na kila linalomhusu yeye. Tena akijitia kulazimisha kuujua undani wake ndipo maongezi hugeuka kuwa uwanja wa vita. "Baba, baba! Huna baba wewe! Mi' nimekuokota tu sehemu. Tena usinikere na makelele juu ya baba'ko," mamaye Kibeka alisema akimtia masingi. Akaongeza kwa kumfunya mashavu kwa nguvu zake zote. Maskini mama Kibeka anaua sisimizi kwa rungu. Kofi likatua shavuni, salamu zikafika hadi masikioni. Filimbi ikalia 'nzeee!' akaziba masikio kuyasikiliza maumivu yake.

***

Alichoropoka katika lindi la mawazo aliposikia dereva anapiga honi kwa nguvu. "Kijana, tumefika. Shuka tena wende ukasome!" Kibeka akajifuta uso uliojawa na huzuni, akashuka garini. Akatazama pande zote za shule, kwa taabu akazifikia hatua zake. Kama hataki, alitembea kwa madoido huku kichwa chini. Katikati ya lango kuu la kuingia darasani kwake, akapigana kikumbo na moja kati ya walimu wa shule.

9 KIBEKA

“*I’m sorry, teacher. I didn’t…*” kabla hajamalizia sentensi yake, mwalimu akamanyamazisha; “*Keep quiet!*” Kibeka akanyamaza. Mwalimu akaanza kumsaili Kibeka kuanzia juu mpaka chini. Hakuelewa inakuwaje anakuja shule bila hata kupaka mafuta. Nguo zake hazijafuliwa vyema. Kibeka aliinamisha kichwa chini. Hakuweza kumtazama ana-kwa-ana mwalimu huyo. “*What is wrong with you?*” mwalimu alimwuliza Kibeka aliyechagua kuwa kimya kwa wakati huo. “*I asked you a question!*” mwalimu akaongeza. Kibeka polepole akainua kichwa na kumtazama mwalimu. Akasema.

“Mama kanipiga!” akashtukia kikofi kidogo kisichoumiza kimetua katika shavu lake. “*English PLEASE*!” mwalimu alifoka. Kibeka akatulia kidogo akisikilizia kofi hilo kutoka kwa mwalimu. “*I had a small fight with my mom*,” Kibeka alijibu. Mwalimu akastaajabu. “*Really?*” akashtukia baada ya kusikia hivyo. “*Yes, teacher*.” Kibeka akajibu kwa chinichini. “*You are an impossible child to raise. No wonder you look like crap! Ptuu*!” mwalimu aliendelea kumsimanga Kibeka. Hakujali. Alishazoea maisha hayo. Zaidi akachagua kunyamaza kimya tu.

“*Go! Go now! Imbecile*!” mwalimu alimsindikiza na maneno ya mabaya Kibeka. “*Thank you, teacher*. Akaingia darasani, akaketi dawati la pili upande wa kushoto. Mwalimu wa somo la kwanza alikuwa hajafika bado. Watoto waliendelea kupiga kelele zao. Kibeka akatoa kitabu chake cha Kiingereza kiitwacho “A Lazy Donkey” kilichoandikwa na Hellen Mwenda, akaanza kudurusu hapa na pale.

Mara akawa anacheka peke yake. *Ni kuhusu kipande cha Punda mzembe jinsi anavyojitia mjanja akibeba mzigo wa chumvi, akafika mtoni, anajitia kudondoka kwa muda mrefu*

akibaki chini, akiinuka, ile chumvi ishayeyuka. Mwenye mali hakutambua hilo mapema. Baadaye sana, akatambua. Siku moja badala ya kumbebesha chumvi, akaweka mchanga. Kufika mtoni, kama kawaida yake, akajibwaga. Jambo lake likawa gumu. Mchanga haukuyeyuka, badala yake, ukawa mzito. Kisa hicho kikamfurahisha sana Kibeka.

Maisha yaliendelea licha ya milima ya hapa na pale. Muda wa masomo uliisha, lakini mwalimu wa mwisho aliagiza wasitoke hadi hapo atakapowaambia kwa sababu alikuwa ana jambo anataka kuwaambia. Kama unavyojua vijana wa rika kati ya miaka kumi na kuendelea, wakiwa peke yao darasani, muda ambao hakuna mwalimu wala masomo, lazima watafanya zogo. Kibeka aliendelea kujisomea kitabu chake. Hakuwa na hili wala lile, mwalimu akavamia ghafla. "*SHUT UP*" alisema kwa sauti kubwa. Punde darasa lote likawa kimya, kama hakukuwa na kilichokuwa kinaendelea. Mwalimu alishika vitabu vyake vitatu vya kufundishia. Alionekana kughadhibika na kile kilichokuwa kinaendelea darasani kwake.

"What do you think you are doing?"

Watoto kimya. Macho yao yamekumbwa na hamaniko kubwa kabisa. Pengine hawakuelewa kupiga kelele darasani si jambo la busara. Pengine utoto. Walihema mno. Vifua vilipanda na kushuka. Macho yakawatoka. Mapigo ya moyo yalitembea kwa kasi mno utasema utachomoka sasa hivi kwa mapigo yake.

"I went outside for two solid minutes then all hell broke loose. Really?" mwalimu alisema huku akikagua nyuso za wanafunzi wake. Pengine angempata kinara wa mazogo ndani ya darasa lake ingesaidia jambo lake, lakini wapi! Kila aliyemtazama, alirusha sura yake kando. Hakutaka kutazamana

naye ana kwa ana. Hofu ya kuitwa mpiga kelele. Akiendelea kutafuta, akamtoa mwanafunzi wa kwanza, aje mbele, wa pili, tatu, nne, wa tano alikuwa Kibeka aliyekuwa akifunga kitabu chake alichokuwa akisoma.

“Kibeka!” aliita kwa sauti. Kibeka akainua kichwa. Akatazama na mwalimu wake pasipo—kupepesa macho. “Stand-up!” mwalimu akaongeza. Kibeka akashangaa. “Me?” aliuliza huku akijioneshea kidole chake cha shahada kifuani kwake. “Yes. You! Stand up and come forward…” kofi kubwa la mshangao lilimpiga Kibeka. “But WHY?” Kibeka alihoji. “I did not make any noise, teacher!” Kibeka akaongeza. Halikumfurahisha mwalimu wake. “I said come forward!” mwalimu alifoka zaidi. “And don’t even think to say any other word…” akatua kwa nukta chache. “You’ll regret it!” akaongeza. Kibeka hakuwa na chaguo lingine tena. Akatoka pale dawatini na kujisogeza mbele alipoambiwa aende. Wanafunzi watano walikuwa wamesimama wakisubiri hatima yao. Mwalimu alikaa kimya.

Akawasaili mmoja baada ya mwingine. Kibeka aliendelea kukaa kimya. Alishikwa na mshangao usiomithilika. Mwalimu aliendelea kujizungusha hadi hapo alipoona inatosha, akaokota bakora yake na kuanza kuita mmoja-mmoja. Zamu ilikuwa kama walivyoitwa. Wa mwisho alikuwa Kibeka. Akatandikwa bakora za mkono zipatazo kumi. Sauti yake haikusikika masikioni mwa watu, lakini huko ndani ya moyo wake ilikuwa ikipiga kelele kubwa sana. Hakuelewa kisa cha kupigwa kwake. Hakuelewa kwanini mwalimu hakutaka kusikia utetezi wake.

“Nimekosa nini mimi Mungu wangu!” alijisemea nafsini. Alipotimiza hilo la kupigwa bila kushiriki katika zogo, akarudi tena kuketi dawatini. Mwalimu hakuwa na habari nao tena.

Akawaruhusu waondoke makwao. Kibeka alitoka polepole huku lindi la mawazo likimkamata ipasavyo fikira zake. Kichwani mwake alizalisha maswali mengi sana yaliyokosa majibu. Hata alipokuja kuwa sawa, *basi* la shule halikuwa tena mbele ya upeo wa macho yake.

Hakushtuka!

Polepole akaanza kutembea akirudi kwao. Bado aliendelea kutafakari namna dunia inavyompiga makofi kila uchao. “Sasa nimekuja duniani kuteseka ama namna gani? WHY always me? What’s wrong did I do to deserve this kind of punishment? When will it come to an end? When? I’m sick of it!” Kibeka alijiuliza maswali mengi sana. Wakati huo tena safari ya miguu ishakolea. Kwa mawazo aliyokuwa nayo, ilibaki punje ndogo tu agongwe na Bajaj.

“We’ mtoto vipi?” dereva wa Bajaj aliwaka huku akishuka kutoka Bajajini. “N’takuzaba makofi mi’,” dereva aliongeza. Kibeka aliendelea kuwa kimya. Akajikunyata tu bila kuongea chochote. “Nisamehe kaka. Sio kusudio langu. Ni bahati mbaya…” kabla hajamaliza, kijana wa Bajaj akamkunja shati lake la shule. Mteja aliyembeba akaona. Akatoka ndani upesi. Hakusubiri tukio liwe kubwa ndipo aingilie.

“We’ dereva hebu mwachie huyo mtoto mara moja!” mteja aliyepakiwa alitoa kauli. Dereva akamwacha. Akamgeukia mteja wake. Hakumwambia kitu, badala yake, akarudi katika usukani wake na kuketi. Dada akamsogelea Kibeka. Akamweka sawa shati lake lililokunjwa. Akamfutafuta kiasi vimichanga vya hapa na pale. Akamwinua kichwa, wakatazamana sasa ana kwa ana.

"Unaelekea wapi?" dada alihoji. Kibeka akajiweka sawa kisha akamjibu. "Manzese Tip Top," Kibeka akajibu. Shule anayosoma iko Sinza Shekilango. "Oh, kumbe sio mbali. Njoo upande nikupeleke hadi hapo barabara ya Morogoro," dada alisema. Kibeka akataka kusita, lakini mwishowe akakubali. Akaingia Bajajini. Dada akamsaili Kibeka kwa ustadi mkubwa. Akamwuliza, "Jina lako ni nani?" lafudhi yake ni ya wanawake waliosomasoma. Si ile ya Uswahilini. Kibeka akahisi hilo. "Ninaitwa Kibeka," kwa upole kabisa alijibu. "Okay! What.." akasita. "Nini hasa kimekupata?" dada alihoji tena kwa Kiswahili. Kibeka akacheka. "It's okay. Speak English, naweza kukuelewa pia!" Kibeka alidakia. Dada akashusha pumzi. Akatoa na tabasamu dogo. Muda huo Bajaji lishaanza safari yake kutokea Shekilango kuja barabara kuu ya Morogoro.

"Nini kimekupata?" dada aliendeleza swali lake.

"Nimepigwa bila sababu."

"Kweli?"

"Ndiyo!"

"Inabidi ukawaelezee wazazi wako."

"Hatojali."

"Una mzazi mmoja tu?"

"Mi' sijui."

"Unaishi na nani?"

"Na mama!"

"Kwanini unasema hatojali?"

"Ni kawaida yake. Hajali lolote litakalonifika mimi—kwake yeye ni sawa tu."

"Oh, jamani. Pole sana!" aliitoa ile Kizungu kabisa. Si kama Mswahili uliyekutana naye mtaani. "Okay… I think there is

something I can do about it," dada alisema. Kibeka akamgeukia kumtazama. "Oh, really?" Kibeka aliuliza kwa mshtuko. "Yeah. There is…" dada alisisitiza kauli yake. "Nitashukuru, madam!" Kibeka akajazia. "Nipe namba ya mama'ko. Nitaongea naye kuhusu wewe na namna bora ya malezi. Sikupendezewa na mwonekano wako wakati unaonekana ni *intelligent*. Akili yako inafanya kazi vizuri sana, lakini malezi yanaweza yasikufikishe unapotaka kwenda," dada alisema huku akitoa simu yake kutoka katika mkoba wake. "Nitajie hizo namba, please!" dada aliongeza. Kibeka akamtajia namba za mama na bibi yake. Akazihifadhi kwa mjina ambayo kwake yatakuwa rahisi kukumbuka.

"Na wewe unaitwa nani, madam?" Kibeka alimwuza dada.

"Oh, me?"

"Yes, you!"

"Ninaitwa Joyce! Niite tu, Madam Joy—itapendeza!"

"Ahsante, madam. Nimefurahi kukutana na wewe!"

Maneno yalimwishia kabisa Kibeka. Nafsi yake ilifurahi kukutana na madam Joy.

***

KITAMBO kikapita, zile tabu alizokuwa akizipitia Kibeka hazikuwahi kukoma. Bahati tu, yule dada anafanya kazi karibu na shule anayosoma Kibeka. Baada ya kupoteana kwa muda, akajaribu kumtafuta Kibeka. Alifika geti la shule na kumwulizia, Mungu bariki ulikuwa muda wa kupata chakula cha mchana, mlinzi akamruhusu dada apite, akamweka katika benchi la wageni akimsubiri Kibeka. Akatumwa mtu kwenda kumwita.

15 KIBEKA

Dakika kadhaa, Kibeka alikuwa mbele ya macho ya dada aliyempa lifti ya Bajaji siku kadhaa zilizopita.

"Madam, shikamoo!" Kibeka alimsalimia huyo dada.

"Marhaba, hujambo?"

"Sijambo, madam Joy!"

"Nimefurahi kukuona, Kibeka!" madam Joy alisema kisha akamgeukia mlinzi. "Naweza kwenda naye lunch hapo nje wakati huu?" madam aliongeza. "Ndiyo. Huu ni muda wao wa kula na kupumzika. Nendeni tu, lakini arudi saa nane sharp!" mlinzi alijibu. "Shukrani! Hatochelewa kurudi…" madam alijibu. Wakatoka. Kibeka sura yake ilijawa na furaha baada ya kumuona madam. Hakutarajia kuonana naye.

"Sikufikiria akilini mwangu kama ningekuja kukuona tena, madam!" Kibeka alisema akichanua tabasamu dogo. "Pole sana. Nilitaka kukuona tena jamani. Halafu nilisoma jina la shule yako katika lebo iliyobandikwa katika mfuko wa shati. Si unajua tena," madam alisema huku akitoa tabasamu. Walifika katika kibanda cha chips, wakaagiza sahani mbili za chips mayai na soda. Da'ika kadhaa mbele, chakula kilikuwa mezani. Hawakuongea sana. Walianza kukishambulia taratibu huku wakisukumia na soda. Kibeka aliendelea kutoa tabasamu mwanana lililokosha moyo wa Joyce kupita kiasi.

"Vipi chakula kitamu?" madam alihoji.

"Ndiyo kitamu!" Kibeka alijibu akisukumia na soda. Madam akajifuta mafuta ya chakula yaliyobaki mdomoni mwake kwa kutumia tishu ndogo zilizokuwa kando ya meza ya chakula. Akasema.

KIBEKA